



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS



TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA

Kumb Na. TCC/S.20/12/C/60

Tarehe: 01 /12/2023

## TANGAZO LA KAZI

Halmashauri ya Jiji la Tanga imepokea kibali cha ajira mbadala kutoka ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma chenye kumb Na. FA.97/228/01 "TEMP"/06 cha tarehe 06 April, 2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga anapenda kuwatangazia nafasi ya kazi kwa watanzania wenye sifa waweze kuomba kama ifuatavyo:-

### 1. DEREVA II - MSHAHARA TGS B: Nafasi 1

#### Sifa za kuajiriwa:

Waombaji wawe na cheti cha mtihani wa kidato cha IV wenye Leseni ya Daraja E au 'C1 ya uendeshaji magari pamoja na uzoefu wa kuendesha magari kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basing Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali. Mafunzo ya ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

#### Kazi na majukumu:


- i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari,
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari,
- vi. Kufanya usafi wa gari na
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri utakavyo elekezwa na Msimamizi wako.

## MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA KWA WAOMBAJI WOTE:

1. Muombaji awe Raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 hadi 45
2. Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya paspoti saizi iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya muombaji na namba ya simu.
3. Waombaji wawe na Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA
4. Waombaji wenyе vyeti vya kidato cha nne na taaluma ambavyo vimepatikana nje ya Nchi wahakikishe vimehakikiwa na Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA). Na Baraza la Elimu ya Ufundı (NACTE).
5. Waombaji waliofukuzwa kazi, kupunguzwa kazi au kuachichwa kazi katika utumishi wa Umma hawaruhuswi.
6. Waombaji ambao hawana sifa wanashauriwa kutokuomba kwa sababu barua zao hazitashughulikiwa
7. Watumishi waliowahi kuajiriwa Serikalini na kupata Cheki Namba hawataajiriwa tena bali wataajiriwa baada ya kupata kibali cha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
8. Juu ya bahasha aandike kazi aliyoomba,
9. Transcript na provision result havipokelewi
10. Maombi yote yatumwe kwa:-

Mkurugenzi wa Jiji,  
09 Barabara ya Hassan Ngwilizi,  
21101 Centra Tanga,  
S.L.P. 178,  
**TANGA**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 14/12/2023 saa 9.30 mchana.**

  
\_\_\_\_\_  
Said M. Majaliwa  
**MKURUGENZI WA JIJI**  
**MKURUGENZI WA JIJI**  
**TANGA**

09 Barabara ya Hassan Ngwilizi, 21101 Central Tanga, S.L.P 178 Tanga, Simu: +27 2643068, +27 2644530/3.  
Nukushi: +255 27 2644141/272647905. Tovuti: [info@tangacc.go.tz](mailto:info@tangacc.go.tz). Tovuti: [www.tangacc.go.tz](http://www.tangacc.go.tz)